# NISHANI YA SARAFU (FEDHA)
# (SANAA NA UFUNDI)

***Maswali***

1. Linganisha kwa ufupi historia ya kubasilisha fedha ukionyesha sababu tatu kwa nini fedha zimeingia katika matumizi na taja angalau aina kumi za fedha za kigeni zilizotumika baada ya sarafu au fedha
2. Eleza kwa kifupi kwa kulinganisha historia ya sarafu na fedha za Karatasi/noti katika nchi yako, hakikisha unataja Tarehe zilipoanza, kiwanda cha kutengenezea sarafu, pia gundua baadhi ya mabadiliko katika madini yaliyomo katika sarafu, pata habari za kuvutia kuhusiana na hayo mabadiliko
3. Elezea namna fedha zinavyosambazwa katika nchi yako
4. Fafanua maana ya maneno haya:-
   a) Alloy
   b) Alama ya mnaanaa – (mint mark)
   c) Altered date – (tareheh zilizobadirishwa)
   d) Obverse – (sehemu ya juu ya sarafu)
   e) Buffered coin – (sarafu za akiba)
   f) Planchet
   g) Cost coin - (sarafu kutupa)
   h) Proof – Nakala
   i) Clad coinage – (watengeneza sarafu bandia)
   j) Receded Edge - paembe zisizotumaini
   k) Commemorative – ya kukumbukwa
   l) Reverse – ya kurudiwa
   m) Die – chapa
   n) Series
   o) Field
   p) Type
   q) Inscription
   r) Whizzed coins
   s) Lehered Edge
   t) Wire edge

5. Eleza sehemu ya juu na ya nyumma ya fedha za daraja la ------- za chini sita za fedha za noti zinazotumika katika nchi yako
6. Elewa namna sarafu zinavyoweka katika madaraja na waksanyaji
7. Kusanya aina mbalimbali ya sarafu katika nchi yako nakala (proof) yakukumbuka – commemorative, shaba – sarafu za ghali hazihitajiki katika ukusanyaji wako.
   a) Pata angalau sarafu moja toka katika kiwanda cha utengenezaji/mahali utakapozipata za aina fulani.
   b) Onyesha na tambua alama za kiwanda kwa kila sarafu.
   c) Onyesha na tambua vifupi vya kila mbunifu wa sarafu
8. Fanya yafuatayo:
   a) Chora machoro mkubwa wa pende zote mbalimbali za sarafu kumi za madaraja mblimbali ya nchi yako ambazo sasa hazisambazwi au kutumika.
   b) Kusanya na tambua aina 25 ya sarafu za kigeni

c) Kusanya seti ya sarafu katika nchi yako zilizotengenezwa katika karne ya 20
d) Kusanya/pata Tarehe/mwaka mtiririko wa sarafu katika nchi yako kuanzia ulipozaliwa, za kukumbukwa, dhahabu za wakala.

**Angalizo**
Maelezo haya yafedha unaweza kuyapata katika idara ya hadina ya taifa ya fedha. Tembelea meneja wa Bank uliza yule anayeweza kukusaidia kupata historia ya fedha za nchi yetu ya Tanzania toka tulipo pata uhuru.

**SARAFU**

1. **Eeleza kwa kifupi historia ya ubadilishanaji wa vitu ukionyesha sababu tatu kwa nini fedha zilitumika na taja angalau aina kumi za fedha zinazotumika badili ya sarafu au fedha.**

   Usitarabu ulipoendelea kuongezeka, wanadamu wakafikia kutambua ugumu uliyojitokeza katika kufanya biashara kwa kubadilishana mali. Ubadilishani ulikuwa ni mtu anakupa kitu na wewe unampa kitu. Mahusiano kati ya watu hawa wawili wanaobadilishana hupangwa kwa namna mbalimbali za madaraja yake. Katika biashara ya kimya mara zingine watu hawakufikia makubaliano mmoja aliacha vitu vyake kwa yule aliyetaka kununua na akaondoka upande mwingine unakuja na kuchukua na kuondoka upande mwingine unakuja na kuchukua vutu vyake na yeye pia kuacha vya kwake kwa mwenzake.

   Kwa waamerika na wakanada, mtindo wa ubadilishaji wa vitu nidyo ulikuwa utaratibu wao mkuu kati ya wafanya biashara na wahindi na kati ya waasisi wenye. Kadri hitaji la fedha lilivyoongezeka swala la kubadilishana likapungua.

   Katika utaratibu huu wa biashara ya kubadilishana kulikuwa na kipimo cha kuliganisha vitu ili kiwe sawa na kile unachotaka kubadilishana, kwa mfano kikapu kimoja nisawa na vizi vingi au kuku mmojani wa Thamani kama uzito furani wa mchele. Vipimo hivi ndivyo vilikuwa vinabadilishana kiwango na mchele kinachotakiwa na kuku mmoja kinaweza kutofautiana kwa sababu kadha na pia na uzalishaji wa mchele. Kuwepo kwa vipimo hivyo hakikizuia kupunguziana bei.

   Mifano ya mabadilishano ya sasa ni sawa na mtu anayetaka kubadili gari la zamani dhidi ya gari jipya. Ukibadilishaji pia unaendeshwa katika ngazi ya kimataifa kati ya nchi na nchi mfano malighafi inaweza ikanunuliwa na nchi Fulani kwa kutengeneza vitu vya nchi vyingine.

   Watu walipotambua ugumu wa kubadilishana vitu, wakaanza kutumia madini kama dhahabu, fedha na vito vya Thamani kama fedha, waanza kutengeneza hayo madini kwa umbo la sarafu.

   Salafu ya kwanza inasemekana ilianza kutengenezwa Asia Monor yapata mwaka 700 B.C/ Karne ya 7 na mfalme wa Lydia au Ioniams. Iliitwa kianzio yaliyokuwa ni madini ambayo hayakuwa yametengenezwa vizuri yaliyowekwa aalama ya chuma kilichotengenezwa kwa nchabganyiko wa dhahabu na fedha iliyoitwa “ELECTRUM”

Wachina pia inasemekana ndiyo watu wa kwanza kutengeneza sarafu. Walizitengeneza kila sarafu kuonyesha kile watakachokileta pamoja na hiyo sarafu, kwa mfano baadhi ya sarafu zilitengenezwa kama umbo la mwanadamu ziliitwa vazi la mwanadamu. Sarafu hizo zilitumika kununulia mavazi.

Katika utaratibu wa kwanza wa fedha Thamani ya sarafu ilipatikana tokana na uzito na usafi wa madini uliyoitengeneza na yaliyotumika. Shekeli iliyotajwa katika Biblia kwa asili ulikuwa ni uzito wa kitu kama ilivyokuwa talanta. Jambo la kuvutia kuhusu maendeleo katika sanaa ya kutengeneza sarafu ilianza na wayunani, sarafu yao ilikuwa na picha ya wajenzi, duni, sanaa na michezo ya kila kipindi cha maisha ya wayunani.

Sarafu nyingi zilikuwa katika umbo baya kwa sababu hii fedha za Karatasi (noti) na chque za banki polepole zilianzishwa badala ya sarafu.

***Ifuatayo hapa chini ni aina za fedha za kigeni***

a) Chumvi
b) Misumari
c) Mikia ya twiga
d) Meno ya Nyangumi
e) Ng'ombe
f) Magamba
g) Mbegu za cocoa
h) Vito vya Thamani
i) Shoka
j) Mawe
k) Kisu
l) Ndoano

**2. Eleza kwa kifupi kwa kulinganisha historia ya sarafu na fedha za Karatasi/noti katika nchi yako. Hakikisha kuwa unataja mwaka waliyoanza kutengeneza. Pia gundua baadhi ya mabadiliko katika madini yaliyotumika kutengenezea sarafu, pata habari za kuvutia kuhusiana na mabadiliko haya.**

Kwa Tanzania nenda hazina au Bank upate habari hizi, kikamilifu.

Fanya umuhimu vijana wa Tanzania waelewe asili ya fedha yao na historia ya fedha Tanzania.

**Kwa Amerika**:
Wahamiaji wa Amerika walitumia aina ya "Wampum" kama fedha. Hii ilikuwa aina ya shanga zilizotengenezwa na wahindi kutokana na aina Fulani ya magamba ya wanyama wa baharini na ziwani. Thamani ya shanga hizi ilitegemea wakati na muda uliyotumika kuzitengeneza.

Dola ya Kihispania pia ilitumuka katika makiloni yao. Sarafu hii iliweza kukatwa katika vipande hivi vidogo viliitwa senti.

Pesa ya kwanza aina ya noti katika makaoloni yao ilitolewa na massachissets mwaka 1690 kulipa majeshi congress ya continental ya pili ilitoa fedha za Karatasi mwaka 1775. hii ilikuwa fedha ya kwanza ya kitaifa ya Karatasi. Fedha aina hii nyingi zilichapishwa Kiasi kwamba zikaonekana kukosa Thamani. Senti za "kituji" zilitolewa 1787 na sarafu ya kwanza ikatorewa na jamhuri ya Marekani mwaka 1792 baraza kuu la congress likaanzisha mpango wa kifedha uliyotumia aina ya mchangayiko wa madini ya aina mbili dhahabu na fedha.

Dola ya dhahabu iliyojaa Kiasi cha punje 24:75 za dhahabu safi na dola ya fedha safi ya Kiasi cha punje 371.25. hii ni wiano wa 1:15 wiano huu ulibadilishwa mwaka 1834 na 1837.

Wakati wa vita ya kitaifa aina kadhaa za fedha za noti zilitumika Marekani ilitoa fedha ya noti ya kwnza mwaka 1861 iliyoitwa :Demand" Greenback. Cheti cha dhahabu na noti za bank ya taifa pia zilianza kutumika wakati huu 1873 mtindo wa kutengeneza sarafu kutumia madini ya aina mbili uliachwa na dhahabu ndiyo ikakubaliwa kama madini ya kutengenezea fedha aina ya sarafu. Baadaye sheria iliagiza pia sarafu aina ya madini ya fedha pia itengenezwe.

Mwaka 1878 katika vita ya dunia nchi nyingi zilifuata mtindo wa taifa Marekani kutengeneza sarafu zao kwa kutumia madini ya dhahabu. Madini yanayotumika kutengeneza sarafu yaliendelea kubadilishwa.

**Angalizo**
Tafuta habari za fedha ya ndani ye nchi yetu ya Tanzania.

3. **Eleza namna fedha zinavyosambazwa katika nchi yetu.**
   Pata habari za fedha ya Tanzania inavyosambazwa.

4. **Eleza maana ya maneno haya:-**
   a) **Alloy** = ni mchanganyiko wa madini zaidi ya moja.
   b) **Altered date** = ni Tarehe/miaka ya uongo juu ya sarafu iliyogeuzwa kufanya sarafu ionekane kuwa ni ya nadra sana au ya Thamani.
   c) **Buffed coin** = ni sarafu iliyosuguliwa au kunakishiwa na kuifanya iwe safi na inayong'ara. Inafanywa hivyo kukufanya wewe ufikiri kuwa haijasambazwa au ni ya hali ya juu kuliko uhalisi wake. Ilea ambayo haijasambazwa kweli haiwezi kunakshiwa.
   d) **Cast coin** = Hizi ni sarafu zinazotengenezwa kwa kumimina ujiuji wa madini katika chombo njia ya kawaida ya kutengeneza sarafu ni kwa kuzipiga chapa.
   e) **Clad coinage** = ni sarafu yenye kitovu na baka la madini ya shaba na nickel au na fedha pande zote. Marekani wanatoa dime, robo ma nusu ya dola hii ilianza mwaka 1965.
   f) **Commemorative** = hii nisarafu iliyotengenezwa kwa kumbukumbu ya kitu Fulani au tukio furani au mtu mashuhuri.
   g) **Die** = chapa hiki ni kifaa kinachotumika kuweka mhuri juu ya pande la madini, chapa hizi zimebuniwa zinazofanya kuvutia juu ya madini zinazpopigwa juu yake.
   h) **Field** = hii ni eneo la uso wa sarafu ambayo hautumiki na wabunifu.

i) **Lettered edge** = huu ni upande wa sarafu uliyo na maandishi yanayotambulisha nchi yenye dhamana na sarafu hiyo
j) **Inscription** = ni herufi zilizo juu ya sarafu.
k) **Mint-mark** = ni alama inayotumika katika sarafu au kutambulisha mahali sarafu ilipotengenezwa mara nyingi ni herufi ndogo.

**Nafasi ya picha**

l) **Components coin** = mali ya mbunifu inayofikiriwa kuonekana kuwa ya muhimu kwa sarafu ambazo hazitumiki kwa mjibu wa sheria.
m) **Obverse** = ni upande wa sarafu uliyo na maandishi ya Tarehe/mwaka
n) **Plan Chet** = ni sehemu isiyo na kitu ya sarafu ambayo inawekwa mhuri.
o) **Proof** = baadhi ya mabaki ya sarafu yaliyoganda wakati wa kuinakshi.
p) **Reeded edge** = hii ni aina ya ncha ya sarafu yenye mikunjo ya mistari ya wima kuzunguka sarafu.

**Nafasi ya mchoro**

q) **Series** = huu ni mtiririko wa matoleo ya sarafu za kila miaka/mwaka, kadri zinavyo chapishwa au kubadilishwa.
r) **Type** = Aina ya safaru zilivyo buniwa.
s) **Whizzed coin** = sarafu ambazo zimeng'arishwa.
t) Wire edge = hii inainuliwa kuzunguka nje ya mzunguko wa sarafu.

5. Elezea uapnde wa sarafu uliyo na maandishi ya fedha aina ya noti za daraja sita za nchi zinazotumika katika nchi yako.
Ubunifu wa fedha ya Kitanzania umekuwa na madaraja mbalimbali katika upande wa maandishi, zingine zina waasisi wa taifa letu la Tanzania, Ikulu, Wanyama mashuhuri wa mbuga za Tanzania.

| **Na** | **Daraja** | **Upande wa mbele** | **Upande wa nyumba** | **mwaka** |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

Elewa ukubwa wa kila noti – sarafu

6. Tambua namna sarafu zinavyowekwa katika madaraja

Hali ya sarafu inaweza kuwekwa katika madaraja kama ifuatavyo:-

**Hafifu:** Sarafu yeyote iliyo na mashimo imepinda imechakaa hata haiwezi kutambuliwa vyema.

**Afashali (fair):** Sarfu yeyote iliyo na uchakavu mwingi lakini bado ule ubunifu wake na maandishi yake bado yapo yanaweza kusomeka.

**Nzuri:** Sarafu ambayo Tarehe, miaka na maandishi yake bado yanaonekana vyema.

**Nzuri sana:** Sarafu ambayo kila kitu chake bado ni safi.

**Njema (fine):** Sarafu ambayo inainyesha uchakavu, vitu vyake vinaonekana lakini alama ya mtengenezaji haipo.

**Njema sana(very fine):** Sarafu hii itaonyesha baadhi ya uchakavu katika mabaka makubwa, yaweza kuwa na alama ya mtengenezaji lakini si sana.

**Njema san asana (extremely fine):** Hii itaonyesha kidogo hali ya kunakishiwa au kusuguliwa katika baka kubwa kwenye maandishi ambayo maandishi yake ya manzo bado yanaonekana.

**Ambayo haijasambazwa (circulated):**Sarafu ,pya ambayo haijasambazwa, haina alama yoyote ya uchakavu.

7. Kusanya aina mbalimbali za sarafu katika nchi yako ya mwaka wowote iliyotengenezwa au kusambazwa, mabaki yaliyo juu ya sarafu, kumbukumbu aalumu, nadra, fedha, sarafu za ghali zisizohitajika katika ukusanyaji wako.
   a) Pata angalau sarafu moja kwa kila toleo.
   b) Onyesha na tambua alama za mahali zilikotengenezwa kama zipo kwa kila sarafu.
   c) Onyesha na tambua vifupisho vya herufi vya kila mbunifu wa sarafu.

      - Hitaji hili kila anayechukua nishani hii kusanya sarafu na fedha zote zilizokwisha tumika katika nchi yetu na baadhi ya sarafu za nchi zingine.
      - Pia kusanya sarafu ulizozikuta toka ulipozaliwa zenye kumbukumbu maalumu, dhahabu na fedha.

8. Fanya kati ya mawili yafuatayo:
   a) Chora mchoro mkubwa wa pande mbili za sarafu au noti za daraja mbalimbali zisizopungua kumi za nchi yako.
      - Wambie wanadarasa wachore picha ya sarafu ya nchi yetu pande zote mbili
      - Pia wachore picha ya noti pande zote mbili.
      - Wakusanye aina 25 za sarafu za nchi mbalimbali, wazifahamu kuwa ni za nchi gani usikusanye zinazofanana.
      - Kusanya sarafu kuanzia mwaka uliyo zaliwa, tambua mwaka ambao sarafu hiyo ilitumika.

**Acha nafasi ya michoro ya sarafu ya Tanzania**